

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARIUTEKELEZAJI WA MAJUMUKU YA MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO  
(e-GA) HADI JANUARI, 2023

**Ndugu Wanahabari,**

Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi wa Taasisi za Umma na utoaji wa huduma kwa wananchi. Lengo la Serikali Mtandao ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika Taasisi za Umma pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa Umma ili huduma hizo zipatikane kwa urahisi, haraka na kwa gharama nafuu kupitia TEHAMA.

**Ndugu Wanahabari,**

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ni Taasisi ya Umma ilioanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya mwaka 2019, ikiwa na majukumu ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali Mtandao, pamoja na kusimamia uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma. Hivyo basi, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ndiyo yenye dhamana ya kusimamia Serikali Mtandao nchini.

**Ndugu Wanahabari,**

Mamlaka imekuwa ikitekeleza jitihada mbalimbali za Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma tangu kuanzishwa kwake mwaka 2012. Awali Taasisi hii ilijulikana kama Wakala ya Serikali Mtandao na baada ya kutungwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao No. 10 ya mwaka 2019, ilipewa hadhi ya Mamlaka.

**Ndugu wanahabari,** Mamlaka imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi yake mikuu sita (6) ambayo ni **Uadilifu, Ubunifu, Kuthamini Wateja, Kufanya kazi kwa Pamoja, Ushirikiano na Weledi.** Utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ni kama ifuatavyo;-

1. **Kusimamia Utekelezaji na Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango, Taratibu na Miongozo ya Serikali Mtandao** kwa kutengeneza Miongozo na Viwango      vya      Serikali      Mtandao      inayopatikana      kupitia <http://www.ega.go.tz//standards>.
2. **Kupitia na Kupitisha Miradi ya TEHAMA ya Taasisi za Umma.** Katika kipindi hiki miradi **340** imepitiwa na kuthibitishwa.
3. **Kuzijengea Uwezo Taasisi za Umma Kutekeleza Jitihada za Serikali Mtandao.** Taasisi mbalimbali za Umma zimevezeshwa kutekeleza jitihada za Serikali Mtandao kwa kutoa Mafunzo mbalimbali kama vile: Usimamizi wa Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali kwa **Taasisi 240**; Kutoa Mafunzo ya Mfumo wa Baruapepe kwa **Taasisi 611**; Kutoa Mafunzo ya Usimamizi wa tovuti kwa **Taasisi 492**.
4. **Kushirikiana na Wadau wa Utekelezaji wa Serikali Mtandao.** Mamlaka inashirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, zikiwemo Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti, Sekta binafsi pamoja na Kuandaa Vikao Kazi vya Mwaka vya Serikali Mtandao ili kuwakutanisha wadau mbalimbali, ambapo katika kikao kazi kilichofanyika Februari mwaka huu, jumla ya **washiriki 1,624 walihudhuria**, ambao ni Wakuu wa Taasisi za Umma, Wataalamu wa TEHAMA na watumiaji wa TEHAMA katika Taasisi za Umma.

Aidha, Mamlaka inashirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kwa lengo la kuhakikisha Serikali Mtandao inaimarika kote Bara na Visiwani. Kupitia ushirikiano huu, Mifumo kadhaa imeboreshwa na inatumiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ). Mifumo hii ni pamoja na: Mfumo wa Barua Pepe Serikalini, Mfumo wa Masjala, Mfumo wa Malipo Zanzibar (ZanMalipo), Mfumo wa Ajira (ZanAjira), e-Wawakilishi na Mfumo wa Ankara za Maji (MAJIIS) kwa ajili ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Pia, Mamlaka inashirikiana na eGAZ katika utoaji wa huduma ya miundombinu ya Serikali mtandao.

5. **Kutoa Ushauri wa Kiufundi kwa Taasisi za Umma** katika utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao na matumizi sahihi na salama ya huduma za Serikali mtandao.
6. **Kukagua, Kupitia, Kutathmini na Kushauri kuhusu hali ya Usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA,** ambapo Mamlaka imefanya tathmini

mbalimbali za usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA, imetambua matishio ya kiusalama mitandaoni na kuainisha hatua za kuchukuwa ili kukabiliana nayo, imeandaa ripoti za usalama wa Mifumo ya TEHAMA ya Taasisi za Umma na kufuutilia utekelezaji wake, imetoa mafunzo mbalimbali kwa Taasisi za Umma kuhusu usalama wa kimtandao, na imeandaa na kutoa miongozo ya kiufundi ya usalama wa Mifumo ya TEHAMA.

## 7. Kufanya Shughuli za Utafiti, ubunifu na Kutoa Mafunzo ya Huduma za Serikali

**Mtandao.** Mamlaka inaratibu tafiti mbalimbali za maendeleo ya jitihada za Serikali mtandao na kubuni Mifumo inayoendana na mahitaji yetu na itakayosaidia kuboresha utendaji kazi katika Taasisi za Umma na utoaji wa huduma kwa Umma, pamoja na kujengea uwezo na kukuza vipaji vya vijana wa kitanzania katika eneo la Serikali mtandao.

## 8. Kujenga Mifumo na Miundombinu Shirikishi na ya Kisekta ya TEHAMA katika Taasisi za Umma

**Ndugu wanahabari,**

Mamlaka imeendelea kusanifu, kujenga na kusimamia uendeshaji wa Mifumo tumizi inayotumiwa katika Taasisi za Umma kwa pamoja (shirikishi). Baadhi ya Mifumo hiyo ni pamoja na:

- ❖ **Mfumo wa baruapepe Serikalini (GMS)** Mfumo huu unaziwezesha Taasisi za Umma kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa usalama, haraka na kwa gharama nafuu ambapo jumla ya Taasisi **616** zinatumia Mfumo huu.
- ❖ **Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office)** jumla ya Taasisi **200** zinatumia Mfumo huu. Aidha Mfumo wa Ofisi Mtandao mbali na kurahisisha utendaji kazi katika Taasisi za Umma pia umesaidia kupunguza matumizi ya karatasi na kwa upande mwingine umesaidia kutunza mazingira na kuokoa fedha za Serikali.
- ❖ **Mfumo wa Utoaji Huduma za Serikali kwa Simu za Mkononi (MGov)** Mfumo wa mGOV umeunganishwa na watoa huduma wote wa simu za mikononi nchini Tanzania, Hadi sasa, Taasisi zaidi ya **275** zimeunganishwa na kuutumia Mfumo wa mGOV kutoa huduma. Baadhi ya huduma hizo ni jumbe fupi yaani SMS za ununuzi wa umeme (LUKU), SMS za huduma za malipo ya Serikali (GePG), Ankara za maji, malipo ya Ardhi, n.k

- ❖ **Mfumo wa Ubadiishanaji Taarifa Serikalini ‘Government Enterprise Service Bus’ (GovESB).** Mfumo huu unawezesha Mifumo mbalimbali ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa, Taasisi zaidi ya 50 zimevezeshwa Mifumo yake kubadilishana taarifa kuitia Mfumo huu. Nitoe wito kwa Taasisi za Umma ambazo hazijaunganisha Mifumo yake katika Mfumo huu, kuunganisha ili ziweze kubadilishana taarifa na Taasisi nyingine pale inapohitajika.
- ❖ **Mfumo wa e- Mikutano** Mfumo huu unaziwezesha Taasisi za Umma kufanya vikao na mikutano kwa njia ya mtandao Hadi kufikia Januari 2023, Taasisi za Umma **192** zimekuwa zikitumia Mfumo huu.

### **Ndugu wanahabari,**

Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Umma, imefanikiwa kutengeneza Mifumo mbalimbali ya kisekta inayotumika katika Taasisi hizo. Baadhi ya Mifumo hiyo ni pamoja na:

- ❖ **Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroniki (GePG) (umetengenezwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango).** Mfumo huu unaimarisha uwazi na udhibiti katika ukusanyaji mapato ya Serikali. Kupitia Mfumo huu, Serikali inao uwezo wa kufahamu mapato yanayoingia kila siku. Mpaka sasa kuna Taasisi na vituo vya kutolea huduma 948 zinatumia Mfumo huu.
- ❖ **Mfumo wa Pamoja wa Utoaji Ankara kwa Mamlaka za Maji Nchini (MAJIIS) (umetengenezwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Maji).** Mfumo huu unarahisisha uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Mamlaka za maji na Bodi za maji za Mabonde nchini Tanzania. Mamlaka za maji 94 zimeunganishwa kwenye Mfumo huu.
- ❖ **Mfumo wa Pamoja wa Uondoshaji wa Shehena Maeneo ya Forodha (TeSWS) (umetengenezwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) pamoja na Taasisi mbalimbali za udhibiti wa shughuli za forodha (Other Government Departments – OGDs))** Mfumo huu umelenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji. Mpaka sasa unatumwa na zaidi ya Mawakala wa forodha (Clearing and Forwarding Agent) 800.
- ❖ **Bunge Mtandao (e-Parliament),** ambao umetengenezwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge. Mfumo huu hutumika kuendesha shughuli za Bunge na kuhifadhi taarifa za Bunge kama vile Miswada na Sheria, Hotuba, Kumbukumbu za vikao vinavyofanyika katika vipindi vya Bunge, Kanzidata ya waheshimiwa wabunge na

majimbo wanayowakilisha. Mfumo huu umewezesha kupunguza kwa kiasi kikubwa sana matumizi ya karatasi Bungeni na kwenye Baraza la Wawakilishi, hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

- ❖ **e-Mrejesho**, (umetengenezwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mfumo huu unawawezesha wananchi kuwasiliana moja kwa moja na Taasisi za Umma kwa njia ya kidigitali, ili kuwasilisha maoni, mapendekezo, maulizo, pongezi au malalamiko yao sambamba na kufuatilia utekelezaji wake ndani ya Taasisi husika. kupitia <https://emrejesho.gov.go.tz>, au kwa kupakua ‘application’ ya e-Mrejesho kwa kutumia simu janja au kupiga namba ya msimbo \*152\*00# kisha chagua namba 9, halafu namba 2 na kisha fuata maelekezo kadiri ya hitaji la mtumiaji. Taasisi za Umma 398 zinatumia Mfumo huu.
- ❖ **Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU)**. Umetengenezwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika) Mfumo huu unarahisisha Ukaguzi, Usimamizi, na Uendeshaji wa vyama vya ushirika ili kuongeza Ufanisi, Uwazi na Uwajibikaji utakaoboresha utendaji na kuchochea mabadiliko ya Kiuchumi. Mikoa 26 imeunganishwa na vyama vya ushirika Zaidi ya 3740 vimeandikishwa kwenye Mfumo.
- ❖ **Mfumo wa Uendeshaji Shughuli za Wakala wa Ununuzi Serikalini (GIMIS)**. Umetengenezwa na Mamlaka kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA). Mfumo huu unarahisisha uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Wakala, pia unaziwezesha Taasisi kupata huduma za ununuzi wa vifaa, mafuta na magari kutoka kwa wakala pamoja na huduma ya ugomboaji na uondoshaji wa mizigo.
- ❖ **Usanifu na Ujenzi wa Tovuti katika Taasisi za Umma**, Mamlaka imesanifu na kutengeneza Tovuti zaidi 350 za Taasisi za Umma, ikiwemo Tovuti Kuu ya Serikali na Tovuti Kuu ya Ajira. Aidha, baada ya Mamlaka kutengeneza Tovuti hizo, ni jukumu la Taasisi husika kuhuisha taarifa za kwenye tovuti zao, Mamlaka inasimamia masuala ya kiufundi katika tovuti hizo.

Aidha, Mamlaka inasimamia uendeshaji na uendelezaji miundombinu ya pamoja ya TEHAMA inayotumiwa na Taasisi mbalimbali za Umma kwa pamoja, hivyo kupunguza gharama kwa Serikali.

### **Ndugu wanahabari,**

Pamoja na kuwa majukumu ya Mamlaka hufanyika kila siku lakini pia Mamlaka hushiriki katika matukio mbalimbali ya kitaifa. Baadhi ya matukio ya kitaifa ambayo Mamlaka imeshiriki kikamilifu na kuleta tija kwa taifa ni pamoja na **Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022**, ambayo ilifanyika kidijitali na kuleta matokeo mazuri pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani kupitia kampeni ya ‘**Royal Tour**’ ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuchapisha matangazo ya kuhamasisha utalii kupitia ukurasa wa GMS na e-office.

### **Ndugu wanahabari,**

Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), imesaidia huduma nyingi za Serikali kupatikana kwa haraka na mahali popote kama ambavyo nimeeleza hapo awali. Aidha, Mamlaka itaendelea kutekeleza azma ya **Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** ya kuhakikisha tunaijenga Serikali ya Kidijiti.

### **Ndugu Wanahabari,**

Katika kuhakikisha tunaijenga Serikali ya Kidijiti, Katika kipindi cha miaka 10 ijayo, Mamlaka itaandaa na kutekeleza mikakati madhubuti ili kuimarisha zaidi utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao kwa kuwa na:

- i. Sehemu moja ambayo huduma mtandao zote zitakuwa zinapatikana.
- ii. Uwezo wa kutumia teknolojia mpya zinazoibuka, hasa zile za akili bandia, sarafu za kidijiti na teknolojia za kifedha, ili kuwezesha maboresho ya kiutendaji katika Taasisi za Umma na utoaji wa huduma kwa Umma.
- iii. Na vijana wa kitanzania wenye uwezo mkubwa wa ubunifu katika utekelezaji wa jitihada za Serikali mtandao.
- iv. Uzalishaji wa vifaa na miundombinu ya TEHAMA (Hardware) ndani ya Tanzania
- v. Mifumo na miundombinu ya Serikali mtandao iliyo bora na imara zaidi.



## **Ndugu wanahabari,**

Ili kufikia yote haya katika kipindi kijacho, Mamlaka imepanga kushughulikia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

- i. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali Mtando kwa Taasisi zote za umma, ikiwa ni pamoja na kupitia na kukagua miradi na Mifumo ya TEHAMA ya kimkakati, kisekta na kitaasisi ili kuhakikisha kuwa imetengenezwa na inatumika kwa kufuata Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo iliyopo na kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake;
- ii. Kupitia na kutathmini hali ya usalama wa Mifumo na Miundombinu ya Serikali Mtando na kuzishauri Taasisi za Umma katika maeneo ya kuboresha, pamoja na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA inafanya kazi wakati wote kwa ufanisi na usalama;
- iii. Kuendelea kuunganisha Mifumo ya Taasisi za Umma kwenye Mfumo wa Serikali wa Kubadilishana Taarifa (Government Enterprise Service Bus - GovESB).
- iv. Kuendeleza shughuli za tafiti na ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA ili kuibua huduma mpya kwa umma na kuwezesha matumizi sahihi ya teknolojia mpya zinazoibuka;
- v. Kujenga mifumo tumizi ya Kisekta kwa kushirikiana na Sekta husika, ili kupunguza wingi wa mifumo na kuboresha utendaji ndani ya sekta; na kuiwezesha kubadilishana Taarifa na mifumo ya sekta nyingine pale inapohitajika.
- vi. Kupanua uwezo wa Mtando wa Mawasiliano Serikalini (Government Network) na kuufikisha katika Wilaya zote nchini ili kurahisisha utekelezaji wa jitihada za serikali mtando na kuwfikishia huduma wananchi wote popote walipo.

### **ASANTENI**

**Imetolewa Na:**

**Mhandisi. Benedict B. Ndomba**

**MKURUGENZI MKUU**

**Mamlaka ya Serikali Mtando (eGA)**

**23/02/2023 - DODOMA**

Mji wa Serikali, Mtaa wa Mtandao, S. L. P. 2833, Dodoma, Simu: +255222129868, Nukushi: +255222129878,  
Barua Pepe: info@ega.go.tz, Mkurugenzi Mkuu: dg@ega.go.tz, Tovuti: www.ega.go.tz

*“Uadilifu na Ubunifu kwa Utoaji Huduma Bora kwa Umma”*

